2. *Hadithi zetu binafsi zinaweza kutofautiana katika muundo binafsi lakini mwishowe sisi wote tuna kitu kimoja cha kawaida.*
3. *Ugonjwa huu wa kawaida au machafuko ni uraibu.*
4. *Tunajua vizuri mambo mawili yanayohusika na uraibu: tamaa ya kutumia na kulazimishwa.*
5. *Tamaa ya kutumia—hilo wazo ambalo huturudisha nyuma mara kwa mara tena kwa dawa fulani ya kulevyia au dawa mbadala, kurudia raha na faraja ambayo tuliwahi kujua.*
6. *¶Kulazimishwa—kwamba mara baada ya kuanza mchakato na dawa ya kwanza, kidonge kimoja, au kinywaji kimoja hatuwezi kuacha kwa nguvu zetu wenyewe.*
7. *Kwa sababu ya unyeti wetu kwa madawa ya kulevyia, tuko katika mtego wa uharibifu ulio na nguvu zaidi kuliko sisi wenyewe.*
8. *¶Tukifika mwisho wa barabara tunaona kwamba hatuwezi kazi tena kama mwanadamu, kwa kutumia au bila kutumia madawa ya kulevyia, sisi wote tunakubwa na janga moja.*
9. *Je, nini kimesalia kufanywa?*
10. *Inaonekana kuna njia mbadala hii: kuendelea hivyo hadi mwisho wa machungu—magereza, taasisi au kifo; au kutafuta njia mpya ya kuishi.*
11. *Katika miaka iliyopita, waraibu wachache sana waliweza kupata chaguo hili.*
12. *Sisi tuna kuwa waaminifu kwetu wenyewe wakati sisi tunakubali kwamba kulevyia kumetushinda sisi na kwamba tunahitaji msaada.*
13. *Ilichukua muda mrefu kukubali kwamba sisi tumeshindwa.*
14. *Tuligundua kwamba hatuponi kimwili, kiakili au kiroho mara moja.*
15. *Hatua ya Nne itatusaidia sisi kuelekea ahueni yetu zaidi kuliko tulivyodhania.*
16. *Wengi wetu tuligundua kwamba hatukuwa wa kutisha wala wa ajabu kama tulivyodhania.*
17. *Tunashangaa kupata kwamba tuna alama nzuri katika hesabu yetu.*
18. *Mtu yeoyote ambaye ana wakati katika Mpango na amefanyia kazi hatua hii atakuambia kwamba hatua ya Nne ilikuwa hatua ya kugeuka katika maisha yao.*
19. *¶Baadhi yetu hufanya makosa ya kukaribia Hatua ya Nne kama ni kukiri jinsi tulivyokuwa waovu—jinsi tumekuwa watu wabaya.*
20. *Kwa njia hii mpya ya maisha, kuwa na hisia ya huzuni inaweza kuwa hatari.*
21. *Hii si madhumuni ya hatua ya Nne.*
22. *Tunajaribu kujinasua wenyewe kutoishi maisha ya ukale, kurudia kuwa bure.*
23. *Sisi tunachukua Hatua ya Nne ili kupata nguvu na busara inayo tuwezesha kukua.*
24. *Tunaweza angalia Hatua ya Nne katika njia nyingi.*
25. *(29). Ni vyema kuwa kabla ya kuanza, sisi kuititia hatua za kwanza tatu na mfadhili.*
26. *(28). ¶Hatua hizi ndizo matayarisho yanayohitajika kuwa na imani na ujasiri wa kuandika hesabu ya maadili bila uoga.*
27. *Sisi tunapata starehe na kuelewa kwetu kwa hatua hizi.*
28. *Sisi wenyewe twajipa fursa ya kuwa na hisia nzuri juu ya kile tunachofanya.*

32. Tumekuwa tukizunguka kwa muda mrefu na hatujaenda popote.
33. Sasa tunaanza hatua hii,bila kukubali hofu yake.
34. Sisi tunaweka kwenye karatasi, kwa kadri ya uwezo wetu sasa.
35. ¶Ni lazima kumalizana na ya kale, si kushikilia tuliyoyafanya.
36. Tunataka kutazama ya kale, kuona jinsi ilivyokuwa na kuiachilia ili tuweze kuishi leo.
37. Matukio ya kale, kwa wengi wetu yamekuwa kama jitu mafichoni.
38. Tumekuwa na uoga wa kuyafichua ya kale kwa kuhofia kile hili jitu laweza kututendea.
39. Hatupaswi kufanya hii peke yetu.
40. Nia yetu na maisha yetu yako katika mikono ya Nguvu ilio Zaidi yetu.
41. ¶Kuandika hesabu hakika na ya uaminifu ilionekana kutowezekana.
42. Ilikuwa, kama tungkuwa tunafanya mambo kwa nguvu zetu wenyewe.
43. Sisi tunachukua muda mfupi kutulia kabla ya kuandika na kuomba nguvu ya kutoogopa na kuwa na uhakika.
44. ¶Katika Hatua ya Nne, tunaanza kujielewa.
45. Sisi tunaandika kuhusu kupungukiwa kwetu kama vile, hukumu, aibu, kujirudia, kujihurumia, chuki, hasira, huzuni, kuvunjika moyo, kuchanganyikiwa, upweke, wasiwasi, usaliti, kukata tamaa, kushindwa, uoga na kujiamini.
46. ¶Sisi tunaandika kwa karatasi mambo yanayo tusumbua sisi hapa na sasa.
47. Sisi huwa na tabia ya kufikiri kinyume, hivyo kuandika kwa karatasi inatupa nafasi ya kuangalia kwa uhakika zaidi nini kinaendelea.
48. ¶Mambo mema lazima pia ieleteke, ikiwa sisi tunataka kupata picha yetu kikamilifu.
13. *Wale amba wameadhiliwa leo wana bahati zaidi.*
14. *Kwa mara ya kwanza katika historia nzima ya mwanadamu, njia rahisi imekuwa ikijithibitisha yenyewe katika maisha ya waraibu wengi.*
15. *Hii inapatikana kwa sisi wote.*
16. *Huu ni mpango rahisi wa kiroho—si kidini, unaojulikana kama Narcotics Anonymous.*
17. ¶*Wakati uraibu wangu ulinileta kwa kiwango cha kukosa uwezo kabisa, ubatilifu na kujisalimisha miaka ishirini na sita iliyopita, kulikuwa hakuna N.A.*
18. *Nilipata A.A. na kwa huo Ushirika nilikutana na waraibu amba walikuwa pia wamepata mpango huu kuwa jibu la tatizo lao.*
19. *Hata hivyo, sisi tulijua kwamba wengi bado walikuwa wanakwenda chini ya barabara ya kukata tamaa, uharibifu na kifo, kwa sababu hawakuweza kujitambua na walevi katika A.A.*
20. *Kitambulisho chao kilikuwa katika ngazi ya dalili dhahiri na si katika eneo la hisia za undani au hisia, ambapo kujielewa huwa tiba ya uponyaji kwa waadhiliwa wote.*
21. *Pamoja na waadhiliwa kadhaa na baadhi ya wanachama wa A.A. amba walikuwa na imani kubwa kwetu na mpango huu, tulianzisha, Julai ya mwaka wa 1953, kile tunachojuwa kwa sasa kama Narcotics Anonymous.*
22. *Tulihisi kwamba sasa mraibu angepata mwanzo wa kujitambulisha vile kila mmoja angehitajika kumshawishi mwenyewe kwamba angeweza kukaa safi, kwa mfano wa wengine amba walikuwa wamepata ahueni kwa miaka mingi.*
23. ¶*Kwamba hii ilikuwa ndio kanuni iliyohitajika, imejidhihirisha kwa miaka inayopita.*
24. *Hiyo lugha isiohusisha maneno lugha ya utambuzi, usahamu na imani, ambayo sisi tunaita kuelewa, iliunda nafasi ambayo tunaweza kujisikia wakati, kugusa ukweli na kutambua maadili ya kiroho ambayo kwa muda mrefu ilipotea kwa wengi wetu.*

25. *Katika mpango wetu wa ahueni sisi ni kuongezeka kwa idadi na kwa nguvu.*
26. *Kamwe hapo mbeleni hakungepatikana waraibu wengi ambao wamekuwa safi kwa hiari yao na katika jamii huru, na kwa uwezo wao kukutana mahali watakapo, ili kudumisha ahueni yao katika ubunifu wa uhuru kamili.*
27. ¶*Hata waraibu walisema haingefanyika kama tulivyopangwa.*
28. *Sisi tuliamini katika mikutano hadharani iliyopangwa; bila kujificha tena kama makundi mengine yalivyojaribu.*
29. *Sisi tuliamini hii ilitofautiana na njia nyngine zote zilizojaribiwa hapo mbeleni na wale waliotetea kujitenga kwa muda mrefu na jamii.*
30. *Tulihisi kwamba ikiwa mraibu angekabili shida yake ya uraibu kila siku kwa mapema angeweza kuwa mwananchi wa maana kwa jamii.*
31. *Hatimaye itatubidi kusimama kwa miguu yetu wenyewe nakukabili maisha kwa uso na kwa masharti yake, hivyo kwa nini tusianze.*
32. *Kwa sababu ya hii, bila shaka, wengi walirudi kutumia na wengi wakapotea kabisa.*
33. *Hata hivyo, wengi walitulia na baadhi wakarudi baada ya kulegea.*
34. *Sehemu ya kutia motisha ni ukweli kwamba wale ambao sasa ni wanachama wetu, wengi wana muda mrefu wakujitenga na matumizi na wana uwezo wa kusaidia mgeni.*
35. *Mtazamo wao, kulingana na maadili ya kiroho ya hatua na mila zetu, ndio nguvu inayoleta umoja zaidi kwa mpango wetu.*
36. *Sasa tunajua kwamba wakati umefika wakati usemi wa kale uliozeeka, “Ukiwa mraibu, daima u mraibu,” kamwe hautavumiliwa na jamii au mraibu mwonyewe.*
37. *Tunapata ahueni.*
38. *Ahueni huanza na kujisalimisha.*
49. *Hii ni ngumu sana kwa wengi wetu, kwa sababu ni vigumu kukubali kwamba sisi tuna wema ndani yetu.*
50. *Hata hivyo, sote tuna wema ndani yetu, mengi ambayo tumeyapata upya katika Mpango huu, kama vile kuwa safi, mawazo wazi, ufahamu wa Mungu, uaminifu kwa wengine, kukubalika, hatua njema, kushirikiana, kuwa tayari, ujasiri, imani, kujali, shukrani, wema na ukarimu.*
51. *Pia, orodha yetu inajumlisha maelezo mengi kuhusu uhusiano.*
52. ¶*Sisi tunatafakali utendaji wetu wa kale na tabia ya sasa hivi ili kuona tutahifadhi nini na nini tunataka kutupilia mbali.*
53. *Hakuna mtu anatulazimisha sisi kutoka kwa taabu yetu.*
54. *Hatua hii ina sifa ya kuwa ngumu; kwa uhakika, ni rahisi sana.*
55. ¶*Sisi tunaandika hesabu ya maadili yetu bila kuzingatia tutayashiriki na nani.*
56. *Sisi twafanya kazi Hatua ya Nne kana kwamba hakuna Hatua ya Tano.*
57. *Tunaweza kuandika peke yetu ama karibu na watu wengine; chochote ni kizuri zaidi kwa mwandishi ni sawa.*
58. *Tunaweza kuandika kwa upana au kama ufupi kama inavyohitajika.*
59. *Mtu aliye na ujuzi anaweza kusaidia na haya.*
60. *Jambo muhimu ni kuandika hesabu ya maadili.*
61. *Kama neno “maadili” lasumbua, tunaweza kuiita hesabu ya mema/mabaya.*
62. ¶*Njia ya kuandika hesabu ni kuandika tu!*
63. *Kufikiria juu ya hesabu, kuzungumza kuhusu suala hilo, kuichambua hutapata kuiandika.*
64. *Sisi hukaa chini na daftari, kuomba mwongozo, kuchukua kalamu zetu na kuanza kuandika.*
65. *Kitu chochote tunachofikiria ni sehemu ya hesabu.*

66. Wakati tunatambua yale machache tunapoteza, na kiasi tunachonufaika, tunaanza hatua hii.
67. ¶Utwala wa msingi wa kidole ngumba ni kwamba tunaweza kuandika kidogo sana, lakini kamwe hatuwezi kuandika zaidi.
68. Hesabu itamfaa mtu binafsi.
69. Pengine hii inaonekana ngumu au chungu.
70. Inaweza kuonekana kama haiwezekani.
71. Tunaweza kuwa na uoga kwamba katika kuwasiliana na hisia zetu tunaweza ashiria mfululizo wa uchungu na hofu.
72. Tunaweza kujisikia kama kuepuka hesabu kwa sababu ya uoga wa kushindwa.
73. Wakati sisi tunapuuza hisia zetu, mvutano unakuwa juu sana kwetu.
74. Uoga wa adhabu itakayojili ni kubwa sana kiasi kwamba inapita uoga wetu wa kushindwa.
75. ¶Hesabu inakuwa afueni, kwa sababu maumivu ya kufanya hivyo ni machache kuliko maumivu ya kutofanya hivyo.
76. Sisi hujifunza kuwa maumivu yanaweza kuwa hamasisho katika kupona.
77. Hivyo, kukabiliana nayo huepuki nayo.
78. Kila mada ya mikutano ya hatua inaonekana kuwa katika Hatua ya Nne au kufanya hesabu ya maadili kila siku.
79. Kupitia mchakato wa hesabu, sisi huweza kukabiliana na mambo yote ambayo yanaweza kutukia.
80. Tunapozidi kuishi kama Mpango wetu, ndivyo Mungu huonekana akituweka katika nafasi ambazo masuala huchipuka,...
81. ...ili tuweze kuandika juu yake.
82. Sisi huanza kufurahia kupona kwetu, kwa sababu tuna njia ya kutatta aibu, hukumu, au hasira.
39. Kutokana na hali hiyo na kuendelea, kila mmoja wetu anakumbushwa kwamba siku moja safi ni siku ya ushindi.
40. Katika Narcotics Anonymous mitazamo yetu, mawazo na athari hubadilika.
41. Sisi tunakuja kutambua kwamba sisi si wageni na kuanza kuelewa na kukubali sisi ni nani.
42. ¶Mradi kumekuwa na watu, uraibu umekuwepo.
43. Kwa upande wetu, uraibu ni tamaa ya kutumia madawa ya kulevyaa ambayo yanatuharibu sisi ikifuatiwa na msukumo ambaao unatulazimisha kuendelea kutumia.
44. Kujiepusha kikamilifu ndio msingi wa njia yetu mpya ya maisha.
45. ¶Hapo zamani, kulikuwa hakuna matumaini kwa mraibu.
46. Katika Narcotics Anonymous, sisi kujifunza kushiriki upweke, hasira na hofu ambayo waraibu huwa nayo kwa kawaida.
47. Mawazo yetu ya zamani ndio yalituvwaka kwa taabu.
48. Sisi hatukulenga kutimiza haja, tulilenga katika utupu na kukosa faida kwa hayo yote.
49. Sisi hawakuweza kukabiliana na mafanikio, hivyo kushindwa ikawa njia ya maisha.
50. Katika ahueni, kushindwa ni vikwazo vyta muda tu badala ya viungo katika msururu usiovunjika.
51. Uaminifu, mawazo wazi na nia ya kubadili ni mitazamo mpya ambayo hutusaidia kukubali makosa yetu na kuomba msaada.
52. Sisi hatulazimishwi kuchukua hatua kinyume na asili yetu na kufanya mambo ambayo sisi hatutaki kufanya.
53. ¶Waraibu wengi hupinga ahueni, na mpango tunaoshiriki pamoja nao huathiri kutumia kwao.
54. Ikiwa mgeni atatuambia kwamba anaweza kuendelea kutumia madawa ya kulevyaa kwa mfumo wowote na kutopata madhara, kuna njia mbili tunaweza kutazama hali hii.

- |     |  |     |  |
|-----|--|-----|--|
| 55. | Uwezekano wa kwanza ni kwamba wao si waraibu.  | 83. | ¶Tuweza pia kuondoa dhiki ambayo ilikuwa ndani yetu.   |
| 56. | Nyingine ni kwamba ugonjwa wao haujatokea wazi kwao na kwamba wao bado wanakana uadhiliwa wao.   | 84. | Kuandika huinua kifuniko kilichofunikia shinikizo letu...  |
| 57. | Kuadhiliwa na kuacha matumizi hypotosha mawazo ya busara, na wageni kwa kawaida huzingatia tofauti badala ya mambo yanayofanana.   | 85. | ...tuone kama tunataka kuitumikia, kuifunikia, au kuitupa nje.   |
| 58. | Wao hutafuta njia za kukanusha ushahidi wa uraibu au kujitoa wenyewe kutoka ahueni.  | 86. | Hatuna haja kutokota ndani yake.   |
| 59. | ¶Wengi wetu tulifanya jambo hilo wakati tulipokuwa wageni, hivyo wakati tunafanya kazi na wengine tunajaribu tusifanya au kusema lolote ambalo litawapa nafasi ya kuendelea kutumia. | 87. | ¶Sisi hukaa chini na karatasi na kalamu na kuomba msaada wa Mungu wetu katika kufafanua kasoro ambazo husababisha maumivu na mateso.                                 |
| 60. | Tunajua kwamba uaminifu na kuelewa ni muhimu.  | 88. | Tunaomba kuwa na ujasiri na kutoogopa na uhakika ili kwamba hesabu hii ikaweza kutusaidia kuweka maisha yetu katika utaratibu.                                       |
| 61. | Kujisalimisha kikamilifu ndio ufunguo wa ahueni, na kujiepusha kikamilifu ndio njia pekee iliyowahi fanya kazi kwetu.  | 89. | Tunapoomba na kuchukua hatua, mambo huwa mazuri kwetu.   |
| 62. | Katika uzoefu wetu, hakuna mraibu ambaye alijisalimisha kikamilifu kwa Mpango huu akashindwa kupata ahueni.  | 90. | ¶Sisi hatutakuwa kamilifu.   |
| 63. | ¶Narcotics Anonymous ni mpango wa kiroho, si wa kidini.  | 91. | Kama tungekuwa kamilifu, sisi hatungekuwa binadamu.  |
| 64. | Mraibu yejote aliye safi ni muujiza, na kuweka muujiza hai ni mchakato unaoendelea wa ufahamu, kujisalimisha na ukuaji.  | 92. | Jambo muhimu ni sisi kufanya bidii zaidi.  |
| 65. | Kwa mraibu, kutotumia ni hali isiyo ya kawaida.  | 93. | Sisi hutumia zana tulizonazo, na kuendelea kupata uwezo wa kustahimilina hisia zetu.   |
| 66. | Sisi hujifunza kuishi safi.  | 94. | Hatutaki kupoteza chochote chenye tumepata; tunataka kuendelea katika Mpango.  |
| 67. | Sisi hujifunza kuwa waaminifu kwetu wenyewe na kufikiri mambo pande zote mbili.  | 95. | Ni uzoefu wetu kwamba hakuna jambo jinsi ya kutafuta na ya uhakika, hakuna hesabu ya athari ya kudumu isipokuwa mara moja ifuatiwe na usawa hakika wa Hatua ya tano. |
| 68. | Kufanya maamuzi huwa ngumu mara ya kwanza.   |     |  |
| 69. | Kabla ya sisi kuwa safi, matendo yetu mengi yaliongozwa na msukumo.  |     |  |

## 1. Hatua Ya Tano

2. "Sisi tulikiri kwa Mungu, kwetu sisi wenyewe, na kwa binadamu mwagine asili halisi ya makosa yetu."
3. Hatua ya tano ndio funguo ya uhuru.
4. Hii inaruhusu sisi kuishi safi, kwa hapa na sasa.
5. Kugawana asili halisi ya makosa yetu, hutuweka huru kuishi.
6. Baada ya kuchukua kwa uhakika Hatua ya Nne, lazima tushughulikie yaliyomo kwa hesabu yetu.
7. Tunaambiwa kwamba tukiendelea kuweka kasoro hizi ndani yetu, zitatuongoza kurudi kutumia.
8. Tunaposhikilia yetu ya kale hatimaye hutufanya wagonjwa na kutuzuia kushiriki sehemu katika njia yetu mpya ya maisha.
9. Kama sisi si waaminifu wakati tunachukua hatua ya tano, tutakuwa na matokeo kinyume kama tuliyopata kutokana na kutoaminika kwa kale.
10. ¶Hatua ya Tano yaashilia kwamba sisi tukiri kwa Mungu, kwetu wenyewe, na kwa binadamu mwagine asili halisi ya makosa yetu.
11. Tumeangalia makosa yetu, tumeona michoro kwa karatasi, na kuanza kuona vipengele vya undani vya ugonjwa wetu.
12. Sasa tunakaa na mtu mwagine na kushiriki hesabu yetu kwa sauti.
13. ¶Nguvu yetu ya Juu itakuwa nasi wakati tunafanya hivi,...
14. ...na itatusaidia kutuweka huru na uoga wa kujikubali sisi wenyewe na binadamu mwagine.
15. Ilionekana si lazima kwa wengine kukubali asili halisi ya makosa yetu kwa Nguvu yetu ya Juu.
16. "Mungu tayari anajua hayo mambo," sisi tulijitolea visababu.

70. Leo, sisi hatujafungwa katika aina hii ya kufikiri.
71. Sisi tuko huru.
72. ¶Kati ahueni yetu, tunaona ni muhimu kukubali ukweli.
73. Mara tunapoweza kufanya hivyo, hatuoni ikiwa na umuhimu kutumia madawa ya kulevyia katika jaribio la kubadili mitizamo yetu.
74. Bila madawa ya kulevyia, tuna nafasi ya kuanza kazi kama watu wenyeye umuhimu, ikiwa sisi kutajikubali wenyewe na dunia hasa kama ilivyo.
75. Tunajifunza kwamba migogoro ni sehemu ya ukweli, na tunajifunza njia mpya ya kutatua migogoro badala ya kuitoroka.
76. Ni sehemu ya asili ya ulimwengu.
77. Tunajifunza kutojihusisha kihisia na matatizo.
78. Tunakabiliana na kilicho mkononi na kujaribu kutolazimisha suluhu.
79. Tumejifunza kwamba kama suluhisho haitendi kazi, basi si ya kiroho.
80. Hapo mbeleni, tulifanya hali rahisi kuwa matatizo; tulifanya milima kutokana na hali tu ndogo.
81. Mawazo yetu bora imetufikisha hapa.
82. Katika ahueni, sisi hujifunza kutegemea Nguvu kubwa zaidi kuliko sisi wenyewe.
83. Hatuna majibu yote au suluhisho, lakini tunaweza kujifunza kuishi bila madawa ya kulevyia.
84. Tunaweza kukaa safi na kufurahia maisha, kama tunakumbuka kuishi "Kwa Leo Tu."
85. ¶Sisi hatujibika kwa ajili ya ugonjwa wetu, bali ni kwa ahueni yetu.
86. Tunapoanza kufanya kazi tulichojifunza, maisha yetu huanza kubadilika na kuwa bora.

87. Sisi hutafuta msaada kutoka kwa waraibu ambaao wanafurahia maisha huru kutoka kwa tamaa ya kutumia madawa ya kulevyo.
88. Hatuhitaji kuelewa Mpango huu ndio upate kufanya kazi.
89. Yote tunahitaji sisi kufanya ni kufuata maelekezo.
90. ¶Sisi hupata misaada kupitia Hatua Kumi na Mbili ambazo ni muhimu kwa ajili ya ahueni, kwa sababu ni njia mpya, ya kiroho ya maisha ambayo inaturuhusu sisi kushiriki katika ahueni yetu wenyewe.
91. ¶Kutoka “siku ya kwanza,” Hatua Kumi na Mbili huwa sehemu ya maisha yetu.
92. Mwanzo, twaweza kujazwa na fikira kinyume, na kuruhusu tu Hatua ya Kwanza kuchukua umiliki.
93. Baadaye, hofu hupungua na tunaweza kutumia zana hizo kikamilifu zaidi na kwa faida kuu kwetu.
94. Tunatambua kwamba hisia za zamani na hofu ni dalili za ugonjwa wetu.
95. Uhuru halisi unawezekana.
96. ¶Tunapozidi kupata ahueni, sisi hupata mtazamo mpya juu ya kuwa safi.
97. Sisi tunafurahia hisia ya kufunguliwa na uhuru kutoka hamu ya kutumia.
98. Tunaona kwamba kila mtu tunayekutana hatimaye ana kitu cha kutoa.
99. Sisi huwa na uwezo wa kupokea na hata kutoa.
100. Maisha yanaweza kuwa safari mpya kwetu.
101. Sisi tunakuja kupata furaha, tabasamu na uhuru.
102. ¶Hakuna mfano wa mraibu anayepata ahueni.
103. Wakati madawa yameondoka na mraibu anaufanyia Mpango kazi, mambo ya ajabu hutokea.
104. Ndoto zilizopotea hufufuliwa na uwezekano mpya hutokea.
17. Ingawaje Yeye tayari anajua, kukiri lazima kutoke kwa midomo yetu wenyewe ili kuwa na ufanisi kweli.
18. Hatua ya Tano si tu kusoma kwa Hatua ya Nne.
19. ¶Kwa miaka mingi, sisi kuliepuka kujiona kama sisi kweli kuliviyokuwa.
20. Tulikuwa na aibu na tulihisi tumetengwa na wengine ulimwenguni.
21. Sasa kwa kuwa tuna aibu yetu ya zamani mateka, tunaweza kuifagia nje ya maisha yetu, ikiwa sisi tutaikabili usoni na kuikiri.
22. Itakuwa yakuhuzunisha kuandika yote chini na kisha kuiweka kwenye kabati.
23. Kasoro hizi hukua katika giza, na kufa katika mwanga wa kuzungumziwa.
24. ¶Kabla ya kuja Narcotics Anonymous, sisi tulihisi kwamba hakuna mtu angeweza kutuelewa au vitu ambavyo sisi tulikuwa tumefanya.
25. Sisi tulioigopa kwamba kama sisi tutajinena wenyewe, bila ya shaka tungekataliwa.
26. Watumiaji wengi wana wasiwasi na hili.
27. Tunatambua kwamba tumekuwa tukipuuza hisia hii.
28. Wanachama wenzetu wana tuelewa sisi.
29. ¶Ni lazima kwa makini kuchagua mtu ambaye atasikia Hatua ya Tano.
30. Ni lazima kuhakikisha kwamba wao wanajua nini tunafanya na kwanini kunafanya hivyo.
31. Ingawa hakuna amri ngumu juu ya mtu wa kuchagua kwetu, ni muhimu kumwamini mtu.
32. Ila tu kuamini kikamilifu katika uadilifu na busara ya mtu inaweza kutusaidia kuwa na nia ya uhakika katika hatua hii.
33. Ingawa hakuna amri ngumu juu ya mtu wa kuchagua kwetu, ni muhimu kumwamini mtu.

34. Tunajua kwamba mlevi mwininge hatakuwa na uwezo wa kutuhukumu sisi na uovu au kutokuelewa.
35. ¶Mara tunapofanya uamuzi na tuko peke yetu na huyo mtu tuliyemchagua kukubali uwazi wetu, tunaendelea, na kutiwa moyo.
36. Tunataka kuwa sahihi, waaminifu na uhakika, tukitambua kwamba hii ni suala la uhai na mauti.
37. ¶Wengine kati yetu wamejaribu kuficha sehemu yetu ya kale, na katika jaribio hili, kujaribu kwa dhati kupata njia rahisi ya kukabiliana na hisia ndani yetu.
38. Tunaweza kufikiri kwamba tumefanya ya kutosha kwa kuandika yote chini, na...
39. ...hii ni kosa hatuwezi kumudu.
40. Hatua hii itadhihirisha nia yetu na matendo yetu jinsi yalivyo.
41. Hatuwezi kutarajia mambo haya kujitangaza yenyewe.
42. Aibu yetu hatimaye tunaishinda, na tunaweza kuepuka hatia siku zijazo.
43. ¶Hatuwezi kupoteza muda.
44. Sisi lazima tuwe hakika.
45. Tunataka kuwaambia ukweli halisi, kikamilifu, haraka iwezekanavyo.
46. Kunayo hatari kwamba sisi huongeza chumvi makosa yetu,...
47. ...na hatari sawia ambayo itapunguza au kujitolea visababu sehemu yetu katika hali ya kale.
48. Hata kama tuko kama jinsi tulivyoingia katika Ushirika wa N.A. bado tunataka “tuonekane wazuri.”
49. ¶Walevi huelekea kuishi maisha ya siri.
50. Kwa miaka mingi, sisi kulifunika chini kujithamini na kujificha nyuma ya miundo isiyo kwamba sisi tuliamini itawenza kuwahadaa watu.
105. Nia yetu kukua kiroho hututia moyo kuendelea.
106. Wakati tunachukua hatua zinazohitajika katika hatua, matokeo yake ni mabadiliko katika maisha yetu.
107. Ni hatua yetu iliyo ya umuhimu.
108. Sisi tunaacha matokeo kwa Nguvu iliyo Zaidi yetu.
109. ¶Ahueni inakuwa mchakato wa kuwasiliana; tunapoteza hofu ya kugusa na ya kuguswa
110. Tunajifunza kuwa tendo rahisi, kama kukumbatia kunaweza kuleta tofauti katika dunia wakati sisi tunajisikia pweke.
111. Sisi tulihisi upendo wa kweli na urafiki wa kweli.
112. ¶Tunajua kwamba sisi hatuna nguvu juu ya ugonjwa ambao hauna tiba, unaendelea na husababisha kifo.
113. Kama hautazuiwa, utazidi zaidi hadi tufe.
114. Hatuwezi kukabiliana na tamaa ya kutumia na kulazimishwa.
115. Njia mbadala tu ni kuacha kutumia na kuanza kujifunza jinsi ya kuishi.
116. Wakati tuko tayari kufuata njia hii na kuchukua fursa ya msaada unaopatikana kwetu, maisha mapya hufunguka kwetu.
117. Kwa njia hii, tunapata ahueni.
118. ¶Leo, tukiwa salama katika upendo wa Ushirika, tunaweza kuangalia mtu mwininge katika jicho na kuwa na shukrani kwa jinsi tulivyo.

*Sura ya Tisa*

**KWA LEO TU—KUISHI KAMA MPANGO**

1. *Jiambie hivi:*  
*KWA LEO TU mawazo yangu yatakuwa kwa ahueni yangu, kuishi na kufurahia maisha bila kutumia madawa.*
2. *KWA LEO TU nitakuwa na imani na mtu katika N.A. ambaye ananiamini na anataka kunisiaidia katika ahueni yangu.*
3. *KWA LEO TU nitakuwa na mpango.*
4. *Nitajaribu kuufuatilia kabisa jinsi ninavyoweza.*
5. *KWA LEO TU kupitia N.A. nitajaribu kupata njia mufti kwa maisha yangu.*
6. *KWA LEO TU sitakuwa na uoga, fikira zangu zitakuwa kwa wale watu ambao ninahusiana na wao, watu ambao hawatumii na wamepata njia mpya ya kuishi.*
7. *Jinsi tu nitakapo fuata hiyo njia, sina chochote cha kuogopa.*
8. *Sisi tunakubali maisha yetu yamekuwa magumu, lakini wakati mwagine tuna tatizo kukiri kwamba tunahitaji msaada.*
9. *Hisia yetu binafsi hutuelekeza kwa matatizo mengi katika ahueni yetu;...*
10. *...tunataka na tunadai mambo kwenda kwa njia yetu.*
11. *Tunapaswa kujua kutohana na uzoefu wetu wa kale kwamba njia yetu ya kufanya mambo haikufanya kazi.*
51. *Kwa bahati mbaya, tulijidanganywa wenyewe zaidi kuliko mtu yeyote.*
52. *Ingawa mara nyingi tulionekana kuvutia na kuwa na ujasiri kwa nje, tulikuwa kweli tukificha mtu mdhaifu na mwenye shida kwa ndani.*
53. *Vificha uso lazima kuondolea.*
54. *Sisi tunashiriki hesabu yetu kama ilivyoandikwa, bila kuruka chochote.*
55. *Tunaendelea kuchambua hatua hii kwa uaminifu na ujuzi mpaka kumalizia.*
56. *Ni faraja kubwa kuondolewa siri zetu zote na kushiriki mzigo wetu wa ukale.*
57. *¶Mara nyingi, tunapo shiriki hatua hii, msikilizaji atashiriki baadhi ya hadithi yake pia, na...*
58. *...sisi hupata kwamba yale mambo yanatuhusu ambayo tulidhani yalikuwa maovu au tofauti si ya kipekee.*
59. *Tunaona, kwa kukubalika na msiri wetu, kwamba sisi tunaweza kukubalika jinsi tulivyo*
60. *¶Kamwe hatuwezi kuwa na uwezo wa kukumbuka makosa yetu yote ya zamani.*
61. *Sisi, hata hivyo, hutoa juhudhi yetu yote.*
62. *Sisi huanza kuhisi uzoefu halisi binafsi wa asili ya kiroho.*
63. *Ambapo mara moja tulikuwa nadharia ya kiroho sisi sasa huanza kuamka kwa ukweli wa kiroho.*
64. *Mtihani huu wa awali wa wenyewe kwa kawaida huonyesha mwenendo wa tabia ambao sisi kwa hakika hatupendi.*
65. *Hata hivyo, kukabiliana na mwenendo huu na kuuleta nje katika wazi hutuwezesha sisi kukabiliana nao kwa mafanikio.*
66. *Hatuwezi kufanya mabadiliko hayo peke yetu.*
67. *Sisi tunahitaji msaada wa Mungu, kama sisi tunavyomwelewa, na Ushirika wa Narcotics Anonymous.*

1. **Hatua Ya Sita**
2. “Tukawa tayari kabisa kwa Mungu apate kuondoa kasoro za tabia zetu.”
3. ¶Kwa nini kuomba kitu kabla ya sisi kuwa tayari kwa ajili yake?
4. Hii itakuwa kuuliza taabu.
5. Hivyo mara nyingi mlevi huwa anatafuta thawabu ya bidii ya kazi bila kufanya kitu chochote.
6. Kuwa na nia ndio jitihada katika hatua ya sita.
7. Jinsi kwa dhati sisihufanya kazi hatua hii itakuwa sawia na tamaa yetu ya mabadiliko.
8. ¶Je sisi kweli tunataka kuwa na kuondoa kinyongo, hasira zetu, uoga wetu?
9. Wengi wetu kushikamana kwa uoga wetu, mashaka, kujichukia wenyeve au chuki kwa sababu huko kuna usalama badia katika maumivu tuliyozoea.
10. Inaonekana salama zaidi kukumbatia kile sisi tunajua kuliko kukiachilia kwa kile hatukijui.
11. ¶Kuruhusu kasoro za tabia yafaa ifanyike kwa maamuzi.
12. Sisi tunateseka kwa sababu madai yake hutudhoofisha.
13. Wakati tulijisifu, sasa kupata kwamba sisi hatuwezi epukana na kiburi.
14. Wale wetu wasio wanyenyekemu huaibishwa.
15. Kama sisi tuna tamaa, tunaona kwamba sisi ni kamwe haturidhiki.
16. Hapo kale tungekwepa na hofu, hasira, kukosa uaminifu au kujihurumia,...
17. ...sasa tunaona pale zinatuzuia uwezo wetu wa kufikiria kwa makini.
18. Kuwa na ubinafsi usiozulika, huwa myororo mharibifu unaotunganisha na tabia zetu mbaya.
13. Kanuni ya kujisalimisha hutuongoza katika njia ya maisha ambayo sisi huteka nguvu kutoka kwa Nguvu kubwa zaidi kuliko sisi wenyeve.
14. Kujisalimisha kwetu kila siku kwa Nguvu ya Juu hutoa msaada tunaohitaji.
15. Kama waraibu tuna shida ya kukubalika ambayo ni muhimu kwa ahueni yetu.
16. Wakati sisi tunakataa kufanyia mazoezi kukubalika, ina maana tunakana imani yetu katika Nguvu iliyo ya Juu.
17. Hofu ni zoezi la ukosefu wa imani.
18. ¶Kujisalimisha mapenzi yetu inatuweka katika kuwasiliana na Nguvu ya Juu ambayo hujaza nafasi tupu ndani yetu ambayo haigeweza kujazwa na chochote.
19. Tulijifunza kumtegemea Mungu kwa msaada wa kila siku.
20. Kuishi kwa leo tu hutuondolea mzigo wa kale na hofu ya baadaye.
21. Tulijifunza kuchukua hatua yoyote muhimu na kuachia matokeo katika mikono ya Nguvu iliyo Juu yetu.
22. ¶Mpango wa Narcotics Anonymous ni wakiroho.
23. Tunapendekeza kwamba kila mtu afanye jaribio la kupata Nguvu ya Juu kumliko kwa kuelewa kwake.
24. Baadhi yetu tuna uzoefu wa kushangaza kiroho, mkubwa nawakutia nguvu kiasili.
25. Kwa watu wengine, mwamko si wa kutabulika.
26. Sisi hupata ahueni katika mazingira ya kukubalika na heshima kwa kila mmoja na kwa imani ya mwengine.
27. Sisi hujaribu kujizuia kujidanganya kwa kiburi na kujiona wenye haki.
28. Kunapoendeleza imani katika maisha yetu ya kila siku, tunaona kwamba Nguvu yetu ya Juu hutujalia na nguvu na uongozi tunaohitaji.

29. ¶Kila mmoja wetu ana uhuru kufanya kazi dhana yetu wenyewe ya Nguvu iliyo ya Juu.
30. Wengi wetu walikuwa na tuhuma na wasiwasi kwa sababu ya kukatishwa tamaa na dini.
31. Kama wanachama wapya, majadiliano ya Mungu tuliosikia katika mikutano ilitusukuma kando.
32. Hadi tulipotafuta majibu yetu wenyewe katika eneo hili, sisi tulikuwa tumenaswa katika mawazo yaliyokusanya kutoka ukale wetu.
33. Watu wasio na msimamo wa imani na watu wasio amini kabisa wakati mwingine huanza kuzungumza na “chochote kile.”
34. Kuna roho au uwezo ambao unaweza kuhisi katika mikutano.
35. Hii kwa wakati mwingine kwa mgeni huwa ndio dhana ya kwanza ya Nguvu iliyo ya Juu.
36. Mawazo ya kale mara nyingi huwa hayajakamilika na yasioridhisha.
37. Kila kitu tunachojuu kinafaa marekebisho, hasa kile sisi tunajua kuhusu ukweli.
38. Tunatafakari mawazo yetu ya kale, ili tuweze kuwa na kuelewa mawazo mapya ambayo huelekeza kwa njia mpya ya maisha.
39. Tunatambua sisi ni binadamu wenyewe ugonjwa wa kimwili, kiakili na kiroho.
40. Wakati tunakubali kwamba uadhiliwa wetu ulisababisha uharibifu wetu wenyewe na kwamba kuna nguvu inapatikana kutusaidia, tunaanza kufanya maendeleo katika kutatua matatizo yetu.
41. ¶Ukosefu wa mabadiliko ya kila siku unaweza kuonekana kwa njia nyingi.
42. Kwa njia ya juhudhi na kuwa na nia wazi sisi huja kutegemea uhusiano wa kila siku na Mungu wa kuelewa kwetu.
43. Kila siku wengi wetu huuliza Nguvu yetu ya Juu kutusaidia kukaa safi, na kila usiku tunatoa shukrani kwa ajili ya zawadi ya ahueni.
19. Kasoro zetu hutunyonya wakati wetu wote na nguvu.
20. ¶Sisi huchunguza hesabu ya hatua ya Nne na kupata mtazamo mzuri wa yale kasoro hizi zinafanya maishani mwetu.
21. Sisi huanza kutamani uhuru kutokana na kasoro hizo.
22. Tunaomba au vinginevyo kuwa tayari, tayari na uwezo wa kuruhusu Mungu kuondoa sifa hizi za uharibifu.
23. Tunahitaji mabadiliko ya utu, kama sisi tunataka kukaa safi.
24. Sisi tunataka mabadiliko.
25. ¶Tunapaswa kukabili tabia mbovu za kale na mawazo timamu.
26. Sisi tunazifahamu na bado sisi tunafanya makosa yale na tunashidwa kuvunja tabia mbaya.
27. Sisi kuangalia Ushirika kwa aina ya maisha ambayo tunataka kwetu wenyewe.
28. Tunawaauliza marafiki zetu, “Je mliachilia kabisa?”
29. Hakika bila upingamizi jibu ni, “Ndiyo, kwa kadri ya uwezo wetu.”
30. Wakati sisi tunaona kasoro zetu maishani na kuzikubali, tunaweza kuziachilia ziondoke na tuendeleze maisha yetu mapya.
31. Tunajifunza kwamba sisi tunakua wakati tunafanya makosa mpya badala ya kurudia yale ya zamani.
32. ¶Wakati sisi tunafanya kazi Hatua ya Sita, ni muhimu kukumbuka kwamba sisi ni binadamu na si lazima tuweke matarajio yasiyowezekana juu yetu wenyewe.
33. Huu ni hatua ya kujitolea.
34. Hiyo ndio kanuni ya kiroho ya Hatua ya Sita.
35. Ni kama kusema kwamba sasa tuko tayari kuchukua mwelekeo wa kiroho.

36. Kwa kuwa sisi ni binadamu, hakika, tutapoteza mwenendo.
37. ¶Uasi ni kasoro ya tabia ambayo hutuharibu sisi hapa.
38. Hatuhitaji kupoteza imani wakati sisi tumekuwa wa kuasi.
39. Kutofautiana au kutovumilia ambako uasi unaweza kudhihirisha kwetu lazima uepukwe kwa kuendelea kuwa na jitihada.
40. Sisi huendelea kuuliza kuwa na kujitolea.
41. Tunaweza kuwa na shaka kwamba Mungu ataona heri kuturehemu au kwamba kitu kitakwenda vibaya.
42. Tunamuuliza mwanachama mwingine ambaye anasema, “Wewe ni hakika uko mahali unapofaa kuwa.”
43. Sisi tunafanya upya utayari wetu kwa kuwa na kasoro zetu kuondolewa.
44. Sisi tunajisalimisha kwa mapendekezo rahisi ambayo Mpango huu unatupa.
45. Hata ingawa sisi hatuko tayari kabisa, tuna elekea njia hiyo.
46. ¶Hatimaye imani, unyenyekevu na kukubali huchukua nafasi ya kiburi na uasi.
47. Sisi huja kujielewa wenyewe.
48. Tunajikuta tunakua katika kukomaa kwa ufahamu.
49. Sisi tunaanza kujisikia vizuri, vile kujitolea kunakua na kuwa matumaini na nafuu.
50. Labda kwa mara ya kwanza, sisi tunaona maono ya maisha yetu mapya.
51. Na haya maoni, sisi tunaweka kujitolea kwetu kwa matendo na kuhamia kwenye Hatua ya Saba.
44. Maisha yetu yanavyo zidi kuwa mazuri, wengi wetu hulegea kiroho, na kuhatarisha kurudia matumizi, tunajikuta katika hatari na kupoteza mwelekeo ambao tumepewa tu ahueni ya kila siku.
45. Huu ni wakati maumivu yetu hutupa tumaini kuchochaea upya marekebisho ya kila siku ya kiroho.
46. Njia moja tunaweza kuendelea kuwasiliana kifahamu, hasa katika nyakati ngumu, ni kuorodhesha mambo ambayo sisi tunajivunia.
47. ¶Wengi wetu tumegundua kwamba kutenga wakati wa utulivu kwetu wenyewe ni muhimu katika kufanya fahamu kuwasiliana na Nguvu yetu ya Juu.
48. Kwa kutuliza akili, kutafakari kunaweza kutuelekeza sisi kwa amani na utulivu.
49. Tulizo hili la akili linaweza fanyika mahali popote, wakati wowote, au namna yoyoye kwa mujibu wa mtu binafsi.
50. ¶Nguvu yetu ya Juu inapatikana kwetu wakati wote.
51. Sisi hupokea mwongozo wakati tunaomba kufahamu mapenzi ya Mungu kwa ajili yetu.
52. Hatua kwa hatua tunapozidi kumtegemea Mungu-kuliko sisi binafsi, kukata tamaa hugeuka kuwa tumaini.
53. Mabadiliko pia inahusisha chanzo kuu ya hofu—yale yasiojulikana.
54. Nguvu yetu ya Juu ni chanzo chetu cha ujasiri tunachohitaji kukabidhi hofu hii.
55. ¶Baadhi ya mambo ni lazima tukubali, na mengine tunaweza kubadilisha.
56. Hekima kujua tofauti huja na ukuaji katika mpango wetu wa kiroho.
57. Tukidumisha hali yetu ya kiroho kila siku, sisi hupata ikiwa rahisi kushughulikia maumivu na kuchanganyikiwa rahisi.
58. Huu ni utulivu wa hisia ambao tunahitaji sana zaidi.
59. Kwa msaada wa Nguvu yetu ya Juu, kamwe hatuhitaji kutumia tena.

60. ¶Mraibu yeote aliye safi ni muujiza.
61. Sisi huweka muujiza huu hai katika ahueni inayoendelea na mtazamo mzuri.
62. Kama, baada ya kipindi cha muda, tunajikuta katika shida na ahueni yetu, labda pengine tumeacha kufanya jambo moja au zaidi ya mambo ambayo ilitusaidia katika hatua za awali za ahueni yetu.
63. ¶Kanuni tatu muhimu za msingi wa kiroho ni Uaminifu, Mawazo-wazi, na Nia ya kujaribu.
64. Sisi tunasema hizi ni UMN za mpango wetu.
65. Uaminifu wa kwanza tunaodhihirisha ni hamu ya kuacha kutumia.
66. Baadaye tunakiri kukosa uwezo kwetu na uthibiti wa maisha yetu.
67. ¶Uaminifu hakika ni chombo muhimu zaidi tulichonacho kujifunza kuishi kwa leo.
68. Ingawa uaminifu ni vigumu kuufanyia mazoezi, una thawabu kuu.
69. Uaminifu ndio tiba kwa fikra zetu zenyen ugonjwa.
70. Imani yetu mpya hufanyika kuwa msingi imara wa ujasiri katika siku zijazo.
71. ¶Kile tulijua kuhusu kuishi wakati tulifika hapa kilikuwa karibu kutuangamiza.
72. Kusimamia maisha yetu wenyewe kulituleta katika mpango wa Narcotics Anonymous.
73. Sisi tulikuja, tukijua kidogo sana kuhusu jinsi ya kuwa na furaha na kufurahia maisha.
74. Wazo jipya haliwezi kupandikizwa kwenye akili iliyofungwa.
75. Kuwa na nia-wazi inaruhusu sisi kusikia kitu ambacho kinaweza kuokoa maisha yetu.
76. Inaruhusu sisi kusikiliza maoni yanayopingana, na kufanya uamuji sisi wenyewe.
77. Kuwa na nia wazi hutuongoza kwenye ufhamu ambao umetukwepa katika maisha yetu.
1. **Hatua ya Saba**
2. "Sisi kwa unyenyekevu Tulimwuliza aondoe upungufu wetu."
3. Kasoro za tabia ni mambo ambayo husababisha maumivu na taabu maishani mwetu.
4. Ikiwa zilichangia kwa afya yetu na furaha, sisi hatungekuja kwa hali kama hiyo ya kukata tamaa.
5. Lazima tungekuwa tayari kuwa na Mungu atuondolee kasoro hizo.
6. ¶Kwa kuwa tumeamua kwamba tunataka Mungu, kama tulivyo Mwelewa, atuondolee hali ya udhaifu au uharibifu wa utu wetu, sisi tumefika katika Hatua ya Saba.
7. Hatungeweza kushughulikia tatizo la maisha sisi wenyewe.
8. Haikuwa mpaka tulipofanya uharibifu halisi wa maisha yetu ndio tuligundua hatuwezi kufanya hivyo peke yetu.
9. Kwa kukubali hivyo, tulifanikiwa kupata mtazamo wa unyenyekevu.
10. Hii ni kiungo muhimu ya Hatua ya saba.
11. Unyenyekevu unachangiwa kwa upana na uaminifu wetu sisi wenyewe,...
12. ...hili ni jambo tumezingatia tangu Hatua ya Kwanza.
13. Sisi tulikubali kulevyia kwetu na kukosa uwezo kwetu.
14. Sisi tulipata nguvu zaidi yetu sisi wenyewe na kujifunza kuitegemea.
15. Sisi tulichunguza maisha yetu na kugundua jinsi sisi kwelitulivyo.
16. Kuwa kweli wanyenyekevu ni kukubali na kwa uaminifu kujaribu kuwa sisi wenyewe.
17. Hakuna hata mmoja wetu ambaye kikamilifu ni mzuri au mbaya kikamilifu.
18. Sisi ni watu ambao wana mema na mabaya na...

- |     |  |     |   |
|-----|--|-----|---|
| 19. | ...cha muhimu zaidi, sisi ni binadamu.   | 78. | Ni kanuni hii inayo turuhusu sisi kushiriki katika majadiliano bila kutoleana hukumu au kungamua haki na makosa.  |
| 20. | ¶Unyenyekevu ni sehemu muhimu, ya kukaa safi, kama vile chakula na maji ni muhimu kwa kukaa hai.   | 79. | Haina haja kuwa wajinga tena kwa kusimamia maadili yasiyo kuwepo.   |
| 21. | Kama kulevyaa kwetu kulivyoendelea, sisi tulizitoa nguvu zetu kutosheleza tamaa zetu.  | 80. | Tumejifunza kwamba ni sawa kutojua majibu yote, hivyo tunaweza kufunzwa na kuishi maisha yetu mapya kwa mafanikio.  |
| 22. | Mahitaji mengine yote hatungeweza kuyafikia.   | 81. | ¶Kuwa na Nia-wazi bila kuwa na utayari, hautatupeleka popote.   |
| 23. | Wakati wote tulitaka kuridhisha tamaa yetu ya msingi.  | 82. | Lazima tuwe tayari kufanya chochote muhimu kupata ahueni.   |
| 24. | ¶Hatua ya saba ni kuchukua hatua, na ni wakati wa kumwomba Mungu atusaidie na ahueni.  | 83. | Kamwe hatujui lini wakati utakuja wakati sisi lazima tuweke juhudzi zote na nguvu tulizo nazo ili kukaa safi.   |
| 25. | Lazima tuelewe kwamba njia yetu ya kufikiria sio njia pekee; watu wengine pia wanaweza kutupa mwelekeo.  | 84. | ¶Uaminifu, kuwa na nia-wazi utayari wa kujaribu, hufanya kazi pamoja.   |
| 26. | Wakati mtu anatuonyesha kasoro yetu, wajibu wetu wa kwanza unaweza kuwa wa kujhiami.   | 85. | Ukosefu wa moja ya kanuni hizi katika mpango wetu binafsi unaweza kusababisha kurudia matumizi, na hakika kufanya ahueni kuwa ngumu na chungu wakati inaweza kuwa rahisi. |
| 27. | Ni lazima kutambua kwamba sisi si wakamilifu.  | 86. | Mpango huu ni sehemu muhimu ya maisha yetu ya kila siku.  |
| 28. | Wakati wote kutakuwa na nafasi ya kukua.   | 87. | Kama si mpango huu wengi wetu tungkuwa wafu au kwenye taasisi.  |
| 29. | Kama sisi kweli tunataka kuwa huru, itabidi tuwe na mtazamo mzuri kwa kile tunaelekezwa.   | 88. | Maoni yetu hubadilika kutoka yale ya ubinafsi hadi ile ya mwanachama.   |
| 30. | Kama upungufu tunaoelewa ni halisi, na tuna nafasi ya kuuondoa, hakika tuta hisi kuwa nafuu.   | 89. | Sisi husisitiza kuweka nyumba yetu kwa mpangilio sababu inatuletea nafuu.   |
| 31. | ¶Baadhi yetu itabidi kwenda kwa magoti yetu kwa hatua hii.   | 90. | Tuna imani katika Nguvu yetu ya Juu kutupa nguvu ili kukidhi mahitaji yetu.   |
| 32. | Baadhi yetu watakuwa na utulivu sana, na wengine kufanya juhudzi kubwa kihisia kuonyesha bidii yao.  | 91. | ¶Njia moja ya kufanya mazoezi kanuni ya UMN ni kwa kuchukua hesabu ya kila siku.  |
| 33. | Neno unyenyekevu linatumika kwa sababu twaendea Nguvu ilio zaidi yetu wenywewe na kuomba uhuru wa kuishi bila upungufu wa njia zetu za kale.               | 92. | Hesabu yetu inaturuhusu sisi kutambua ukuaji wetu wa kila siku.   |
| 34. | Wengi wetu tu tayari kufanya hivyo bila upingamizi, juu ya imani pofu, kwa sababu sisi ni wagonjwa kwa yale tumekuwa tukifanya na jinsi sisi tunavyo hisi. | 93. | Hatupaswi kusahau wema wetu katika kujitahidi kuondoa kasoro zetu.  |
| 35. | Chochote kinachofanya kazi, sisi tutafuata.  | 94. | Ule udanganyifu wa kale na ubinafsi unaweza kubadilishwa na kanuni za kiroho.   |

95. ¶Kukaa safi ni hatua ya kwanza katika kukabiliana na maisha.
96. Wakati tunafanya mazoezi kukubalika, maisha yetu huwa rahisi.
97. Wakati matatizo yanajitokeza, tunatarajia kuwa tumejihami na zana za mpango.
98. Sisi kwa uaminifu tunafaa kusalimisha ubinaksi na uharibifu wetu wenyewe.
99. Siku za kale sisi tuliamini kukata tamaa kungetupa nguvu ya kuishi.
100. Sasa tunakubali wajibu kwa ajili ya matatizo yetu na kuona kwamba sisi tuna kuwajibika kwa ajili ya suluhu yetu.
101. ¶Kama waraibu wanaopata ahueni, tuna mengi ya kushukuru.
102. Wakati kasoro zetu zinaondolewa, tuko huru kuwa kile tunaweza.
103. Tunaibuka watu wapya na kujifahamu sisi wenyewe na uwezo wa kuchukua nafasi yetu katika dunia.
104. ¶Katika kuishi kama hatua, tunaanza kuachilia ubinaksi wetu.
105. Tunaomba Nguvu yetu ya Juu katuondolea hofu yetu ya kukabiliana nasi wenyewe na maisha.
106. Tunajitambua upya wenyewe kwa kufanya kazi hatua na kutumia zana za ahueni.
107. Tunajiona kuwa tofauti.
108. Haiba yetu hubadilika.
109. Sisi huwa watu wenye hisia, wenye uwezo wa kukabiliana ipasavyo na maisha.
110. Sisi tunaweka maisha ya kiroho kwanza na kujifunza kutumia uvumilivu, subira na unyenyekevu katika mambo yetu ya kila siku.
111. ¶Watu wengine katika maisha yetu hutusaidia kuendeleza uaminifu na mitazamo ya upendo, tunadai machache na kutoa zaidi.
112. Hasira huzidi kupungua polepole na kusameheana huja kwa urahisi.
36. ¶Hii ni njia yetu kwa kukua kiroho.
37. Sisi tunabadilika kila siku...
38. ...hatua kwa hatua, kwa uhakika na kwa umakini tunajivuta wenyewe kutoka kwa kutengwa na upweke wa uadhilwa na kuingia katika utawala wa maisha.
39. Hii haiji kwa kudhania, lakini ni kwa hatua na maombi.
40. Lengo kuu la Hatua ya Saba ni kutoka nje yetu sisi wenyewe na kujitahidi kufikia mapenzi ya Nguvu yetu ya Juu.
41. ¶Kama sisi tutakuwa na kutojali na kushindwa kuelewa maana ya kiroho ya hatua hii, sisi tunaweza kufufua matatizo ya zamani.
42. Hatari moja ni kuwa wakali sana kwetu wenyewe.
43. ¶Kushiriki na wahadhiliwa wengine katika ahueni itatusaidia kuepuka kuwa wakali sana kwetu wenyewe.
44. Kukubali kasoro za wengine kunaweza kutusaidia kuwa wanyenyekevu na kupata njia kwa ajili ya kasoro zetu wenyewe kuondolewa.
45. Mungu mara nyingi hufanya kazi na wale ambao hujali sana ahueni ili kutusaidia kutambua upungufu wetu.
46. ¶Tumebaini kuwa unyenyekevu una sehemu kubwa katika mpango huu na njia yetu mpya ya maisha.
47. Sisi huchukua hesabu yetu, na huwa tayari kuruhusu Mungu kuondoa kasoro zetu za tabia; na kwa unyenyekevu Kumwomba atuondolee upungufu wetu.
48. Hii ni njia yetu ya kukua kiroho, na sisi tunataka kuendelea.
49. Tuko tayari kwa Hatua ya Nane.

## 1. Hatua ya Nane

2. “*Sisi tulifanya orodha ya watu wote tuliokuwa tumewadhuru, na kuwa tayari kupatana nao wote.*”
3. ¶Hatua hii ni mtihani kwa unyenyekevu wetu mpya tuliuopata.
4. Kusudi letu ni kupata uhuru kutochana na hatia tulioishi nayo mpaka sasa,...
5. ...tunataka kuangalia ulimwengu katika jicho bila ukali wala hofu.
6. ¶Je, sisi tuko tayari kufanya orodha ya watu wote tuliokuwa tumedhuru ili kuondoa hofu na hatia ambayo maisha ya kale yametushikia
7. Uzoefu wetu unatuambia kwamba ni lazima tuwe tayari kabla hii hatua.ifanye kazi kwetu.
8. ¶Hatua ya Nane si rahisi, inadai aina mpya ya uaminifu kuhusu uhusiano wetu na watu wengine.
9. Hatua ya Nane inaanza mpango wa kusamehe wengine na labda tunasamehewa nao, kujisamehe wenyewe, na kujifunza jinsi ya kuishi katika dunia.
10. Wakati, sisi hatimaye tunafikia hii hatua, tuko tayari kuelewa badala ya kueleweka.
11. Tunaweza kuishi na kuishi rahisi zaidi wakati sisi tunajua maeneo ambapo sisi tunahitaji marekebisho.
12. Inaonekana ngumu sasa, lakini wakati tumetimiza hayo, tunashangaan mbona hatukifanya kitambo.
13. ¶Tunahitaji uaminifu halisi kabla ya kutengeneza orodha sahihi.
14. Katika kuijandaa kufanya orodha ya Hatua ya Nane, ni muhimu kufanua madhara.
15. Ufanuzi moja ya madhara ni uharibifu wa kimwili au kiakili.
16. Ufanuzi mwengine wa madhara ni kusababisha maumivu, mateso au hasara.
17. Uharibifu unaweza kusababishwa na kitu ambacho kimesemwa, au kufanyika au kutofanywa, na,...

113. Tunajifunza kuhusu upendo kutoka kwa wanachama wa Narcotics Anonymous.
114. Kupitia upendo tunaopokea katika Ushirika wetu sisi huanza kuhi upendo, hisia ambayo kabisa ni geni kwetu kutochana na maisha yetu ya ukale.
115. ¶Heshima yetu binafsi ilitudhibiti katika kila aina ya njia ya hila.
116. Hasira ni jawabu kwa hali yetu ya sasa.
117. Majuto ni kurudi kuishi hali ya ukale tena na tena katika akili zetu, na hofu ni jawabu letu la siku za usoni.
118. Tunahitaji kuwa tayari kuruhusu Mungu kuondoa hizi kasoro ambazo hulemaza ukuaji wa kiroho.
119. ¶Mawazo mapya yanapatikana kwetu kwa njia ya kuzungumzia uzoefu wetu wa kuishi.
120. Kufanya mazoezi kwa bidii miongozo rahisi katika sura hii, sisi hupata ahueni kila siku.
121. Kanuni ya mpango huuda mpangilio wa maisha yetu.
122. ¶Kutochana na kutengwa kwa uraibu wetu, sisi hupata ushirika wa watu wenyewe nia moja ya kupata ahueni.
123. N.A. ni kama merikebu ya uokoaji katika bahari ya kutengwa, kukata tamaa na uharibifu na machafuko.
124. Imani yetu, nguvu na matumaini huja kutoka kwa kushiriki ahueni yao na kutochana na uhusiano wetu na Mungu wa kuelewa kwetu.
125. Mara ya kwanza tunahisi ugumu kushiriki hisia zetu.
126. Sehemu ya maumivu ya uraibu inakatizwa katika kushiriki huku.
127. Kama tunajikuta katika mahali pambaya au kuhi shida ikija, sisi tutamuita mtu au kwenda kwa mkutano.
128. Sisi hujifunza kutafuta msaada kabla ya kufanya maamuzi magumu.

129. Kwa kunyenyeka na kuomba msaada, tunaweza kustahimili nyakati.za ugumu.
130. Kama mimi siwezi, tunaweza!
131. Kwa njia hii sisi hupata nguvu tunayohitaji wakati tunaihitaji zaidi.
132. Sisi huunda utangamano tunaposhiriki rasilimali zetu za kiroho na kiakili.
133. ¶Kushiriki katika mikutano mara kwa mara na moja-kwa-moja na waraibu wanaopata ahueni inatusaidia kukaa safi.
134. Kuhudhuria mikutano inatukumbusha jinsi ilivyo kuwa mpya na asili ya maendeleo ya ugonjwa wetu.
